

**HOTUBA YA MKURUGENZI MKUU WA MAMLAKA YA HALI YA HEWA  
TANZANIA KWENYE MKUTANO WA WADAU KUJADILI JINSI UTABIRI  
WA MVUA ZA MSIMU WA OKTOBA-DISEMBA, 2018  
UTAKAVYOWEZA KUTUMIKA KATIKA SEKTA MBALIMBALI (SECTOR  
IMPACT ASSESSMENT OF OND, 2018 SEASONAL RAINFALL).  
ULIYOFANYIKA LAW SCHOOL OF TANZANIA, DAR ES SALAAM,  
TAREHE 03 SEPTEMBER, 2018.**

**Ndugu Wakurugenzi wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.**

**Wafanyakazi, Wageni Waalikwa;**

**Mabibi na Mabwana;**

Naenda kuchukuwa fursa hii kumshukuru mwenyezi mungu kwa kutujaalia afya njema na kutuwezesha kujumuika hapa siku ya leo.

Pia nachukua nafasi hii kuwakaribisha wote katika mkutano huu muhimu kuhusu KUJADILI JINSI UTABIRI WA MVUA ZA MSIMU WA OKTOBA-DISEMBA, 2018 UTAKAVYOWEZA KUTUMIKA KATIKA SEKTA MBALIMBALI (SECTOR IMPACT ASSESSMENT OF OND, 2018 SEASONAL RAINFALL).

Binafasi nimefurahi kupata fursa hii kujumuika nanyi katika mkutano huu ambayo ni sehemu ya kubadilishana uzoefu kati ya wataalamu wa mamlaka ya hali ya hewa na wale kutoka sekta mbalimbali. Kukutana

huku ni muhimu katika kujenga na kuimarisha utoaji wa huduma za hali ya hewa kwa jamii.

Kama mjuavyo, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania ni ofisi pekee inayotoa huduma za utabiri wa hali ya hewa kwa jamii kwa niaba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mamlaka hii inahusika kutoa tahadhari za majanga yatokanayo na hali ya hewa yanayoathiri sana watu na mali zao. Majanga hayo ni pamoja na mvua kubwa na upepo mkali hasa katika kipindi cha misimu ya mvua; upepo mkali na mawimbi makubwa baharini na ziwani wakati wa kipupwe. Hali hii inaleta changamoto kubwa kwa wananchi hususan wakulima, wavuvi, wafugaji na wasafirishaji.

Aidha tunajua kuwa, msimu unaokuja wa Oktoba hadi Desember 2018 ni msimu wa mvua katika baadhi ya maeneo hapa nchini hasa yale yanayopata misimu miwili ya mvua, vile vile ni msimu wa kilimo katika maeneo hayo; hivyo ni muhimu kwa wanamchi na watumiaji wengine wa taarifa za hali ya hewa kupata taarifa sahihi na kwa wakati ili kuweza kujipanga na kujiandaa kabla ya msimu kuanza.

Mamlaka na Serikali kwa ujumla inatambua madhara yatokanayo na hali mbaya ya hewa nchini. Serikali imekuwa ikijitahidi kuijengea uwezo Mamlaka ya Hali ya Hewa kadri iwezekanavyo ili iweze kutekeleza vizuri majukumu yake na watumiaji wa taarifa hizo wazipate mapema na kufanya maamuzi sahihi kwa wakati muafaka.

Katika mkutano huu, wadau kutoka sekta mbalimbali wanapata fursa ya kuona utabiri wa hali ya hewa wa msimu wa Oktoba hadi Disemba na kuchangia juu ya athari zitakazopatikana katika sekta zao kutokana na utabiri huu.

Hivyo ni matarajio yangu kuwa, kutoka katika kikao hiki muhimu, watazania watapata utabiri ulio kamilika wa hali ya hewa inayotarajiwa na pia athari zinazoweza kutokana na hali hiyo inayotarajiwa na hivyo kupata wasaa wa kujipanga ili kupunguza au kuepusha kabisa madhara.

### **Ndugu Wadau, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana**

Kazi inayofanyika leo pia ni sehemu ya utekelezaji wa mradi wa HHHHH unaofadhiliwa na shirika la umoja wa mataifa la FAO ambapo ni matokeo ya juhudi za pamoja kati ya FAO na nchi wanachama wa kuhakikisha huduma bora na usalama wa chakula. Juhudi hizo zinakwenda sambamba na na dhamira na dira ya mamlaka ya hali ya hewa ya kuhakikisha huduma za hali ya hewa zinatolewa kwa ubora unaokidhi mahitaji katika kiwango cha juu kabisa.

Kama nilivyoieleza hapo awali kwamba taarifa za hali ya hewa ni muhimu kwa usalama wa watu na mali katika ustawi wa jamii, hivyo ni dhahili kwamba wadau wa taaluma mbalimbali ambazo kwa njia moja au nyingine zinahusiana na hali ya hewa wanao mchango

mkubwa katika kusaidia kueleweka kwa taarifa za utabiri hivyo kusaidia wananchi kuondoa au kupunguza madhara.

Ufuatiliaji wa taarifa za hali ya hewa ni muhimu na unalenga katika kulinda maisha ya watu na mali zao. Aidha taarifa za hali ya hewa zinalenga kusaidia katika kufikia malengo ya Mpango wa Maendeleo ya Milenia ya Umoja wa Mataifa (MDGs), hususan katika maeneo ya uhakika wa chakula na upunguzaji wa makali ya umasikini, kupunguza athari zitokanazo na majanga yanayosababishwa na hali mbaya ya hewa. Hivyo, lengo la mkutano huu wa kikazi ni kuongeza mchango wa wataalam juu ya matumizi ya taarifa za hali ya hewa kwa sekta mbalimbali, kukusanya maoni na ushauri kutoka katika makundi ya wadau yanayotumia taarifa za hali ya hewa. Mkutano huu pia utatumika kuelimisha wadau na hatimaye jamii kwa ujumla juu ya tafsiri bora na sahihi za utabiri wa Mvua za msimu wa vuli kwa sekta mbalimbali.

### **Ndugu Wadau, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana**

Kwa hayo machache, napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru wadau kutoka sekta mbalimbali kwa kutenga muda wenu na kuitikia mwito wa kushiriki katika mkutano huu muhimu na natamka rasmi kuwa mkutano huu umefunguliwa.

Nawatakia kila la kheri.

ASANTENI SANA